

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

LAANA YA KIFO

Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.—Mwanzo 2:17.

Hapo mwanzo Mungu aliumba Shamba la Edeni. Shamba hili lilikuwa la ajabu na liliumbwa ili kuwafurahisha Adamu na Hawa. Hapa ni mahali ambapo Mungu angefanya ushirika na hawa viumbe wake. Bwana Mungu akaweka mti wa uzima hapo, pamoja na mti wa ujuzi wa wa mema na mabaya, humo katikati mwa shamba hilo (Mwanzo 2:9). Kama Adamu na Hawa wangaliendelea kula kutoka kwa mti huo wa uzima, afya yao na ukakamavu wao wa maisha ungeweza kudumishwa. Viumbe hawa waliumbwa nafsi zao zikiwa hai, nafsi zenye uwezo wa kuishi milele, naye Mungu akatoa nafasi kwao wa kuweza kuishi milele mwilini. Lakini Mungu pia akawaamuru wasile kutoka kwa mti ule wa ujuzi wa mema na mabaya. Adhabu ya kutofuata agizo hilo lingekuwa ni wao kupatwa na mauti. Basi Mungu akamuumba mwanadamu akiwa kiumbe chenye uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu tabia zake mwenyewe, akampatia uwezo wa kufanya maamuzi yake. Hili ni jambo la lazima ikiwa mtu atakuwa na uwezo wa kuchagua kile ambacho yeze mwenyewe atachagua kukipenda.

Lakini Adamu na Hawa wakaanguka katika majaribu ambayo yaliletwa na adui na wakala matunda kutoka kwa mti amba waliwa wameonywa wasile. Wakati walifanya dhambi hiyo macho yao ikafunguka wakatambua mema na mabaya (Mwanzo 3:6-7). Ufahamu huo ukamwondolea mwanadamu hali ambayo alikuwa ameumbwa nayo, yaani hali ya kiumbe kisichokuwa na hatia wala dosari. Kabla ya tendo hilo la uasi Adamu

na Hawa walikuwa viumbe wasio na hatia, viumbe wenye usafi wa kiroho.

Basi Mungu akawa mwaminifu kwa neno lake, kama ambavyo mpaka sasa Yeye ni mwaminifu, na kama atakavyokuwa mwaminifu hata katika siku za usoni. Lile tangazo ambalo Mungu alifanya shambani kuhusiana na kifo likatimia. Je, hiki kifo kilikuwa cha aina gani? Laana ya kifo ilikuwa laana ya aina mbili—laana ya kiroho na ya kimwili.

Basi kukatokea kifo cha kiroho ambacho kililetu utengano kati ya Mungu na mwanadamu. Mungu ni Mungu mtakatifu na kamwe hawezu kuwa mshirika na kile ambacho sio kitakatifu. Ushirika wa kiroho na uhusiano amba ulikuwako kati ya Mungu na mwanadamu ukavunjika kutokana na dhambi hiyo ya Adamu na Hawa. Roho ya mwanadamu nayo ikaingia uharibifu kwa ajili ya ufahamu wa mema na mabaya, uharibifu amba uliendelezwa na kizazi cha Adamu. Hata katika siku zetu watoto hawana haja ya kufundishwa kufanya mabaya kwa maana mvuto amba wao huzaliwa nao huwa ni mvuto wa dhambi. Ndiposa Mfalme Daudi akanena kuhusu jambo hili katika Zaburi 51:5 “Tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alinichukua mimba hatiani.” Hapa Daudi anazungumza kutokana na yeze kutambua hali ya asili yake ya dhambi, ambayo alikuwa nayo tangu mwanzo. Kanuni hii ya kuzaliwa dhambini wakati mwingu hujulikana kama “dhambi ya kiasili,” maanake mvuto wa dhambi amba kila mwandamu huleta ulimwenguni wakati yeze anapozaliwa.

Kumekuwa na migogoro mingi ya kidini na migawanyiko mikubwa kuhusu chanzo au kupidishwa kwa asili ya dhambi ambayo ilianza katika Shamba la Edeni na ambayo imepitishwa na kufikia vizazi tofauti tofauti.

(Endelea katika Ukurasa 2)



“Shetani... anajaribu kufanya Wakristo kuishi kwa woga na kufanya juu chini kuua, kuiba, na hata kuangamiza maisha yetu ya kiroho.”

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Raho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

Lakini mjadala unapoisha kila mshirika anayetafuta ukweli anastahili kutambua ukweli wa Warumi 3:23, "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Tabia na mvuto alio nao mwanadamu ambaye hajakombolewa ni wa kutenda matendo ya dhambi na ya kimwili. Lakini kuititia kwa damu ya Yesu na utakaso wa nguvu zake Raho Mtakatifu mwanadamu anawenza kurudishiwa uhusiano bora na Mungu. Na hata ingawa mvuto wa dhambi utaendelea kuweko (kutokana na uwezo wa kufanya maamuzi ambao wanadamu walipewa), mvuto

mkubwa zaidi ambao mtu aliyekombolewa huwa nao ni kwa mambo ya utakatifu.



**"Shetani amewataka
ninyi apate kuwapepete
kama vile ngano; lakini
nimekuombea wewe ili
imani yako isipungue."**

ni ya milele Mungu alitangaza kwamba "kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi" (Mwanzo 3:19). Kwa kweli huu sio mpango ambao Mungu alikuwa nao hapo mwanzoni, ulizuka baada ya Adamu kutenda dhambi, "Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima" (Mwanzo 3:24). Tangu wakati Adamu na Hawa walipofukuzwa shambani na wakaacha kula kutoka kwa mti ule wa uzima miili yao iliacha kufanya upya na badala yake miili (yao) ikaanza kudhoofika. Yaonekana kama kwamba kuendelea kudumu kwa mwili wa mwanadamu kulitegemea ye ye kuzidi kula kutoka kwa mti wa uzima. Ubora wa tunda hilo la mti wa uzima ndilo ambao ulipatia miili ya wanadamu hao nguvu na kuidumisha dhidi ya kuzoroteka. Lakini tangu Adamu kutenda dhambi miaka ya maisha yake ya kimwili na wanadamu wenzake humu duniani yalikatika.

Laana ya dhambi ilileta kifo cha kiroho na kimwili. "Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23). Kifo cha kiroho na kifo cha kimwili zilitokana na dhambi ya Adamu ambayo ilipitishwa kwa watu wote. Kifo cha kiroho ni kutenganishwa au kutengwa kwa roho ya mtu kutoka kwa Mungu, kutokana na ukosefu wa utakatifu. Kifo cha kimwili (maanake kukatika kwa shughuli za mwili wa mwanadamu na utendaji kazi wake) ni jambo ambalo lilianza kutokana na kuanguka kwa mwanadamu huyo. Kwa kweli tangazo la kifo lilikuwa moja, lakini matokeo yake yalikuwa ya aina mbili tofauti, nayo madhara yake yakasambaa kote kote. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwashimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuititia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unawenza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

Tahariri



Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. —1 Wakorintho 15:21

Kifo chaa kiroho na cha kimwili kiliingia maishani mwa mwanadamu kuptitia kwa dhambi ya Adamu; lakini tunahitaji kumshukuru Mungu kwa maana kwa njia ya Yesu Kristo kifo kiliweza kushindwa. Maisha ya kibinadamu yaliingia kwa njia ya Adamu, lakini maisha ya milele yakaja kwa njia ya Yesu Kristo. Kwa sasa dhambi na mauti hazina nguvu juu ya mwanadamu kwa sabau laana ilivunjwa kuptitia kifo na kufufuka kwa Bwana wetu.

Katika robo hii ya mwaka jalida hili la Ukweli wa Injili linashughulikiwa thiolojia kuhusu kifo cha kwanza na cha pili, na kufufuka kwa kwanza na kwa pili. Mimi nimeomba, nijakifunza, nikafanya utafiti mwingi kuhusiana na maswala haya. Kuna mafundisho mengi ya uwongo ambayo yanafundishwa kuhusu masomo haya, mafundisho ambayo yako kinyume na mafundisho ya kimsingi ya Kristo. Hata wakati nilipofanya utafiti wa maandishi mengi ya kale ambayo yaliandikwa na washirika wa Kanisa la Mungu nilikutana na mawazo tofauti tofauti kuhusiana na maeleo kamili ya mambo haya na maana yake. Wengi wa washirika wa Kanisa la Mungu ambao waliandika kuhusu maswala haya walishikilia kwamba kifo cha kwanza ni kile cha kimwili ilhali wengine walisema kwamba hiki ni kifo cha kiroho ambacho kilitukia hapo katika Shamba la Edeni. Lakini mafundisho hayo yote mawili yamo sambamba na mwelekeo wa kawaida wa mafundisho ya Biblia.

Basi sasa nimefikia matokeo ya uchunguzi wangu na ningependa kusema kwamba mimi nina amani ya kiroho na ya kimawazo kuptitia kwa njia ya Neno la Mungu ninaposema kwamba chanzo cha "Kifo cha Kwanza" ni tangazo lile la kimsingi ambalo Mungu alitamka na ambalo lilikuwa ni adhabu ya uasi wa mwanadamu. Tangazo hilo MOJA likawa na matokeo ya aina MBILI—ya kimwili na ya kiroho. Naye Kristo akasuluuhisha laana hiyo moja (ambayo ilikuwa katika sehemu mbili) kwa njia ya ufufuo wa kwanza na wa pili.

Mimi mwenyewewe nimepata uvuvio na kupokea mwangaza kuptitia kwa maandiko ambayo tumeyashirikisha katika toleo hili. Ombi langu ni kwamba kila msomi atapata changamoto la kuweza kufufuliwa kiroho kwa njia ya Kristo na kupata maonyo kuhusiana na tangazo la mwisho na ambalo ni la pili kuhusiana na kifo ambacho bado hakijawadia na ambacho kitafika kwa wale ambao hawajamwamini; kifo ambacho kitawadia siku ya hukumu itakopofika. Lakini shukrani zetu zote ni kwake Mungu kwa sababu jehanamu haina nguvu juu ya wale ambao tayari washafufuliwa kiroho.

Michael W. Smith

Julai 2019



Tutembelee

www.thegospeltruth.org

ili kujianidikisha na
kupata jarida

za mbele.

KIFO CHA KWANZA NA CHA PILI—NA UFUFUO WA KWANZA NA WA PILI

Ufufuo wa Kwanza (wa Kiroho)



Kifo cha Kwanza
(Cha Kiroho na cha Kimwili)

Mwanzo 2:17
Warumi 5:12
Warumi 6:23



Ufunuo 20:6
Yohana 11:25
Waefeso 2:1

Waliokombolewa

Ufufo wa Pili (wa Kimwili)



Ufunuo 20:11-13
Yohana 5:28



Hukumu



Warumi 14:10

Uzima wa Milele (Mbinguni)



Ufunuo 7:13-17
Ufunuo 21:4-7



Kifo cha Pili
(Jehanamu)

Ufunuo 20:14-15
Ufunuo 21:8

Njia Nyembamba
Njia Panya
Wale ambao Hawajakombolewa

Ufufuo wa Kimwili




Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: Kifo cha Kwanza, cha Pili, na Pia Ufufuo

Somo la Biblia: Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu.—Ufunuo 20:6a

Muhstasari: Dhambi ambayo Adamu alifanya katika Shamba la Edeni iliwaletea wanadamu laana ya kifo. Kifo hiki ambacho kilikuwa ni cha kwanza kilikuwa cha kimwili na pia cha kiroho. Yesu Kristo alikuja ulimwenguni ili kwa njia ya kufufuka kwake wanadamu waweze kupata tiba ya matokeo haya mawili ambayo yalitokana na dhambi. Ufufuo wa kwanza ni wa kiroho ambao hupatikana kwa njia ya wokovu, nao ufufuo wa pili ni ule wa kimwili ambao utatokea mwishoni mwa nyakati. Hata ingawa kwa sasa kuna tiba ya kifo cha kwanza, wale ambao hawampokei Kristo na kushiriki ufufuo huo wa kiroho hawatakuwa na tiba kutokana na laana ya kifo cha pili ambacho kitakuwa ni cha mwisho na ambacho ni hukumu ya milele huko jehanamu



I. Matokeo ya Dhambi katika Shamba la Edeni

- A. Mwanzo 2:9 Miti aina mbili spesheli katika Shamba la Edeni.
- B. Mwanzo 2:16-17 Faida na matokeo ya miti hiyo miwili.

II. Kifo cha Aina Mbili

- A. Warumi 5:12 Kifo ni matokeo ya dhambi ya Adamu.
- B. Mwanzo 3:19 Kifo cha kimwili.
- C. Mwanzo 3:22,24 Adamu anatengwa kutoka kwa mti wa uzima.
- D. Warumi 6:23 Mshahara wa dhambi ni mauti.
- E. Mwanzo 3:5-7 Hali ya kutokuwa na hatia inapotea kutokana na dhambi.
- F. Zaburi 51:5 Upotovu wa mwanadamu.
- G. Isaya 59:2 Dhambi inatutenganisha na Mungu.

III. Kifo cha Kiroho na Ufufuo wa Kiroho

- A. Luka 15:24 Mwana mpotevu.
- B. Yohana 5:24-25 Hali ya kuondoka kutoka kifoni na kupata uzima.
- C. Waefesi 2:1,5-6 Wale waliokuwa wamekuwa dhambini walihuishwa.
- D. Warumi 5:8-21 Kifo kiliingia kupitia kwa Adamu. Wokovu uliingia kupitia kwa Kristo.

- E. Yohana 11:25-26 Kuishi kwa njia yake Kristo.

IV. Kifo cha Kimwili na Ufufuo wa Kimwili

- A. Yohana 5:28-29 Ufufuo kutoka kwa wafu.
- B. 1 Wakorintho 15:26 Kifo ni adui wa mwisho.
- C. 1 Wakorintho 15:42-57 Ufufuo wa kimwili.

V. Kifo cha Pili

- A. Ufunuo 20:12-15 Kifo cha pili ni hukumu ya milele.
- B. Mathayo 22:13 Kulia na kusaga meno.
- C. Luka 16:23-24 Jehanamu ni mahali pa mateso.
- D. Marko 9:43-44 Moto huo hautawahi kuzimwa.

VI. Washiriki wa Kifo cha Pili

- A. Ufunuo 21:8 Wenye dhambi.
- B. Ufunuo 2:11 Mwenye kushinda hatapata madhara yoyote.
- C. Ufunuo 20:6 Kifo hiki hakitakuwa na nguvu juu ya waliookoka.

Tamati

Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima. —Ufunuo 2:10b

UONGO ULIOKO KATIKA MAFUNDISHO YA USALAMA WA MILELE

Kifo kilikuwa ni adhabu ya dhambi ambayo chanzo chake ni uasi wa wanadamu katika Shamba la Edeni? Kifo hicho “cha kwanza” kilikuwa cha aina mbili, kwa sababu kiliunganisha kifo cha kiroho na cha kimwili. Tangazo la kifo lilikuwa la mpito kwa sababu Yesu Kristo alitoa njia sambamba ambayo kwake roho ya mwanadamu ingeweza kufufuliwa ili aweze kupata maisha mapya na kuweza kurudishiwa uhusiano na Mungu. Zaidi ya hayo, nguvu za kifo cha kimwili ilivunjwa na Kristo, na ndiposa kutakuwako na ufufuo mwengine wa kimwili, wakati muda wa dunia utakapofikia kikomo.

Ufufuo wa Kwanza (wa Kiroho)

“Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni yeze aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya

hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu.” (Ufunuo 20:6). Ufufuo wa kwanza ni ufufuo wa kiroho ambao hutokea wakati mwenye dhambi ametubu dhambi zake na kufanywa hai kwa njia ya Yesu Kristo. Yesu alifafanua kuhusu swala hili katika mfano wake wa mwana mpotevu, ambaye aliondoka nyumbani na kuvunja uhusiano wake na baba yake. Wakati kijana huyu mpotevu aliporudi nyumbani baba yake alifurahi na kusema “Kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia” (Luka 15:24). Mwana huyu hakuwa amekufa kimwili lakini kiroho alikuwa amekufa. Waliokufa kiroho wanafanywa hai tena kupitia ufufuo wa kiroho.”



“Adhabu ya

kifo cha kiroho ikaondolewa kwa njia ya ufufuo wa kiroho. Basi sehemu ya kifo hicho ambayo ni ya kiroho ikabatilishwa kwa njia ya ufufuo wa kiroho. Jambo hili linaonyeshwa vizuri kupitia kwa ubatizo wa maji, ambapo tunafufuliwa kutoka kwa wafu ili tuenende kwa njia ya uzima mpya (Warumi 6:4-5). Hata ingawa sio maji yanatuokoa ubatizo ni ishara ya ufufuo ambao unafanyika wakati mtu ameokolewa na damu yake Yesu. Ufufuo huu wa kiroho ambao ni kukombolewa kwa roho ya mwanadamu kutoka kwa kifo kinachosababishwa na dhambi, na hata akaweza kupata uzima mpya katika Kristo, ndio ambao unajulikana kama ufufo wa kwanza.

naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu” (Waefeso 2:5-6).

Kifo cha Kiroho Chabatilishwa

Warumi 5:8-21 inafundisha kwa njia ya wazi kabisa kwamba dhambi na kifo kiliwajia watu wote kupitia kwa dhambi yake Adamu; lakini kuhesabiwa haki kulijiri kupitia kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Sasa mwanadamu anaweza kupatanishwa na Mungu kupitia kwa kifo kufufuka kwa Mwanae. Ndiposa imenakiliwa: “Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele” (Yohana 11:25-26). Adhabu ya kifo cha kiroho ikaondolewa kwa njia ya ufufuo wa kiroho. Basi sehemu ya kifo hicho ambayo ni ya kiroho ikabatilishwa kwa njia ya ufufuo wa kiroho. Jambo hili linaonyeshwa vizuri kupitia kwa ubatizo wa maji, ambapo tunafufuliwa kutoka kwa wafu ili tuenende kwa njia ya uzima mpya (Warumi 6:4-5). Hata ingawa sio maji yanatuokoa ubatizo ni ishara ya ufufuo ambao unafanyika wakati mtu ameokolewa na damu yake Yesu. Ufufuo huu wa kiroho ambao ni kukombolewa kwa roho ya mwanadamu kutoka kwa kifo kinachosababishwa na dhambi, na hata akaweza kupata uzima mpya katika Kristo, ndio ambao unajulikana kama ufufo wa kwanza.

Ufufuo wa Pili (wa Kimwili)

Kuna sehemu ya pili ya kifo cha kwanza ambayo ni sehemu ya kimwili. Yesu alikuja ili kutuletea uzima tele na ndiposa akatoa nafasi ya kubatilishwa kabisa kwa kile kifo cha kwanza. Roho ya mwanadamu ikafufuliwa na kupata uzima mpya kwa njia ya ufufo huo wa kwanza, nao mwili wa kifo utafufuliwa katika ufufo wa pili. “Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote walioomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu” (Yohana 5:28-29). Ufufuo wa kimwili utakuweko katika siku sijazo, “Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti” (1 Wakorintho 15:26). Yesu alifafulu dhidi ya kifo na akashinda kwa njia ya ufufuo wake. Na wakati Yesu atakaporudi kutakuweko na ufufuo wa kimwili, na wakati huo kila kiumbe kitasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu.


(Endelea katika Ukurasa 6)

“Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeze aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. Amin, amin, nawaambia, Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai.” (Yohana 5:24-25). Yesu hakuwa akisema kuhusu kifo cha kimwili, na pia hakuwa akizungumza kuhusu ufufuo wa wa kimwili; badala yake Yeye alikuwa akinena kuhusu hali ya kiroho ya mwenye dhambi ambaye sasa amekuwa muumini na hivyo kupata ujuzi wa uzima kupitia kwa Mwana wake Mungu. “Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja

(Inaendelea kutoka Ukarasa 5)

Mwili huu amba ni wa uharibifu na wa kibinadamu utafufuliwa na kufanywa usiwe wenyewe kuharibika, wenyewe kudumu milele. Ndiposa kifo kitamezwa na ushindi huo! (1 Wakorintho 15:42-57).

“Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa” (1 Wakorintho 15:21-22). Ufupo huu wa pili ndio unaojulikana kama ufufuo wa pili. Tangazo la kwanza limekuwa mwavuli amba mwanadamu tangu wakati wa Adamu; lakini kwa njia ya Kristo kukapatikana ufufuo wa aina mbili amba unamaliza na kuzibatilisha nguvu aina mbili za kifo cha kwanza. Ufufuo wa kwanza ni wokovu, nao ufufuo wa pili ni ufufuo wa kimwili kutoka kwa wafu.



“Lakini kuna tangazo lingine la kifo litakalotoka kwa Mungu na ambalo ni la mwisho na la milele; basi kwa kifo hicho hakutakuwa na tiba ambayo itawahi kutolewa ya kumwezesha mtu kuokoka adhabu ya kifo (hicho).”

yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha

uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto” (Ufuno 20:12-15). Kifo cha pili kitatokea katika siku ya hukumu kwa wote amba wamekataa kukombolewa kutokana na nguvu za kile kifo cha kwanza kupitia kwa Yesu Kristo.

Hakutakuwa na Tiba ya Kifo cha Pili

Jehanamu ni mahali pa mateso (Luka 16:23-24) na giza nyingi; hapo kutakuwa na giza la njie na “kilio na kusaga meno” (Mathayo 22:13). Jehanamu ni makao ya milele ambako “funza wao hafi, wala moto hauzimiki” (Marko 9:43-44). Hakutakuwa na mwisho wa mateso ya kiroho na kimwili na uchungu kutokana na kifo hiki cha pili. Pia hakutakuwa na tumaini la kupata mwokozi au mkombozi mwingine kwa maana hakutakuwa na tiba ya kifo hicho.

Wote wasiomcha Mungu na amba hawakukombolewa watakuwa chini ya himaya na nguvu ambazo hazididimii za kifo hicho cha pili. “Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili” (Ufunuo 21:8).

Okoka, Ili Uweze Kuepuka Kifo Hicho cha Pili

Tunahitaji kumshukuru Mungu kwa sababu kuna ukombozi kutoka kwa kifo cha pili kwa njia ya Yesu Kristo. Hata ingawa wanadamu wote walikuwa chini ya nguvu za kifo cha kwanza kiroho na kimwili kutokana na dhambi ya Adamu, watu wote sasa wanaweza kukombolewa kutokana na nguvu za kifo cha kwanza kupitia kwa Yesu Kristo. Kifo cha pili (ambacho kitawafanya wanadamu kudumu milele jehanamu) hakitakuwa na nguvu juu ya wale ambao tayari wameshiriki ufufuo wa kiroho. “Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni ye ye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu” (Ufunuo 20:6a).

Kipawa cha Yesu Kristo kinabadilisha matokeo ya kifo cha kwanza, na kipawa hicho kinatuhakikishia uhuru kamili kutokana na kifo cha pili. Hebu basi tukubali utakaso ambao Yesu alitupatia kutoka dhambini ili tuweze kupokea wokovu huu mkuu. Hebu basi kila siku tufuate nyayo za Bwana na tuishi maisha matakatifu ambayo yanampendeza Baba. Mbingu inawangojea wale ambao wamepitia ujuzi wa ufufuo huu wa ajabu wa kiroho, wale ambao tayari wametoka kwa mautini na kufika katika uzima. Ahadi yake Bwana haitingisiki na kwa kweli ni ya hakika: “Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili” (Ufunuo 2:11b). ■

Maswali na Majibu

Je, 1 Wathesalonike 4:13-18 inafundisha kwamba ufufuo wa watakatifu utafanyika wakati tofauti na ufufuo wa wenyе dhambi? Je, ufufuo wa kimwili utakuwa wa aina mbili tofauti.

Kutakuwa na ufufuo mmoja tu wa (ki)mwili wakati ambapo wafu watatoka makaburini mwao. Yohana 5:28-29 inafundisha jambo hili kwa njia wazi kabisa, "Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu." Hata ingawa kuna manabii wa uongo ambao wanafundisha kwamba kutakuwa na ufufuo wa aina mbili, Yesu mwenyewe alisema kwamba watakatifu na wasiokuwa watakatifu watafufuliwa wakati mmoja au katika kipindi kimoja. Hili ni jambo ambalo ni kinyume na mafundisho ya utawala wa miaka elfu moja.

1 Wathesalonike 4:16 inafundisha kwamba wakati Bwana atakaporudi "waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." Baadaye katika mstari wa 17 inasema "Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele." Andiko hili linasema kwa njia ya wazi kabisa jambo ambalo litatendeka kwa watakatifu wakati Bwana atakaporudi. Kwa kweli andiko lenyewe halineni kuhusu hatma ya waovu, na pia halineni kuhusu ufufuo wao, wakati ambapo watapata adhabu ambayo Yesu alisema kuhusu katika Yohana sura ya 5. Wathesalonike wa Kwanza 4:13-18 iliandikwa ile kuwapa moyo wale ambao walikuwa na tumaini katika Kristo (mstari wa 13) na pia kuwafariji watakatifu (mstari wa 18).

Kutakuwa na ufufuo mmoja wa kimwili wa watu wote wakati ambapo Yesu Kristo atarudi.

Tafadhali toa maelezo kuhusu Ufufuo 20:5-6 katika muktadha wa kile ambacho kimeandikwa kuhusiana na ile miaka elfu.

Andiko lenyewe linasema hivi: "Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Huo ndio ufufuo wa kwanza. Heri, na mtakatifu, ni ye ye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu" (Ufunuo 20:5-6).



Katika kufanya utangulizi wa andiko hili hebu tukumbuke yale mafundisho rahisi ya Yesu ambayo yanapatikana katika Yohana 5:24-29, kuhusu ufufuo ambao utakuwa wa aina mbili. Moja ya ufufuo huo ulianza wakati wa Yesu, na huo ulikuwa ufufuo wa kiroho (Saa inakuja, na SASA ipo), ilhalii ufufuo wa pili utakuwa katika siku za usoni na utakuwa wa kimwili (saa INAKUJA).

Basi hebu tutazame swalii ambalo tunakabiliana nalo hapa. Ufunuo 20:5-6 haisemi kuhusu ufufuo wa miili, bali inazungumza kuhusu ufufuo wa roho ambazo zilikuwa zimeuawa kwa ajili ya imani yao katika utawala wa Ukataliki wa Kirumi na pia katika miaka ya Uprotestanti. Andiko hili kamwe halifundishi wala kuashiria kuhusu utawala wa miaka elfu moja duniani. Mstari wa 4 unazungumza kuhusu "roho zao waliokatwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu." Ni roho hizi, na sio miili ya watakatifu, ndizo ambazo zilikuwa zinatawala paradiso wakati wa mafundisho mengi ya uongo na hadaa nyangi. Kipindi ambacho kilijaa giza ambalo liliadhiri hata siku zilizofuata. Kabla ya kipindi hiki cha miaka elfu moja, ambacho kimesemwa kwa njia ya kimfano kumaanisha kipindi kirefu, kanisa la kwanza lilioneckana duniani likiwa lenye ushindi mkubwa. Lakini katika kipindi hicho cha mafundisho ya uongo kanisa ambalo lilikuwa duniani lilikuwa kanisa la uongo. Ndiposa kukatolewa ufufuo huo wa kanisa ambalo lilikuwa lingali linatawala huko paradiso wakati mafundisho ya uongo yalikuwa yanatawala duniani. Roho ambazo zilikuwa zikitawala ni zile za watu ambao walikuwa tayari wamepata uujuzi wa nguvu ambao ulibadilisha maisha yao, nguvu ambazo zilitokana na ufufuo wa kwanza, kwani watu hawa walipokea wokovu wakiwa wangali humu duniani kabla ya kuuawa kwa ajili ya imani yao.

Ufufuo wa kwanza haukuwa tu wa wale ambao waliuawa kwa ajili ya imani yao katika siku zilizopita, lakini ufufuo wenyewe ndio uliwezesha roho zao kutawala pamoja na Kristo, badala ya wao kulemewa na nguvu za kifo cha pili, ambacho ndicho hukumu ya milele. Wakati miaka hiyo elfu moja (kipindi kirefu) ilipokwisha kanisa likaonekana tena duniani likiwa lenye nguvu na ushindi.



JE, WAJUA?

Ufuno 22:1-2 inafafanua kuhusu mti wa uzima ambao ulikuwa ukimea katika pande zote mbili za mto wa uzima, mto ambao chanzo chake kilikuwa ni kiti cha enzi cha Mungu. Mstari wa tatu unasema kwamba "hapatakuwa na laana yo yote tena." Mtoto wa Mungu ana nafasi ya kuufikia mti huo wa uzima hata katika nyakati tunazoishi na kuweza kufika mahali ambapo kifo cha kiroho hakipo tena. Lakini katika upande ule mwengine wa mto, kwa muda ambao hauna kikomo, mti wa uzima unaendelea kunawiri kwa njia ya mafumbo, mahali ambapo watakatifu wote wataweza kukula matunda yake, na kupata uzima wa milele, hapo kwenye uwepo wa Mwana Kondo wa Mungu.



TUTABADILISHWA

Angalieni, nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadilika.—1 Wakorintho 15:51

Mtume Paulo aliwaandikia watakatifu wa Korintho kuwashimiza waendelee kuwa waaminifu kwa Bwana. Akawaambia kwamba baadhi yao watakuwa tayari washakufa ilhali wengine watakuwa wangali hai wakati Kristo atakaporudi. "Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na ucharibifu, nasi tutabadilika" (1 Wakorintho 15:52).

Ewe mtoto wa Mungu, jua kwamba mabadiliko yaja! Miili yetu itazeeka na hata wengi wetu watafika mahali pa kukosa afya bora. Mwishowe mwili huu hufa na kurudi mavumbini ambako ndiko ulikotoka. Mambo haya yote yanatokana na laana ya kifo ambayo iliwekwa juu yetu kama wanadamu katika Shamba la Edeni. Lakini laana hiyo ni ya mpito kwa yule ambaye ni mtoto wa Mungu kwa sababu Yesu alishinda kifo na kuvunjilia mbali nguvu za laana. Mungu asifiwe sana!



Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

Wakati Yesu atakaporudi wafu watafufuka kutoka makaburini mwao, na watu wa tabaka, lugha na vizazi tofauti tofauti watabadilishwa. Ufufuo mkuu wa nguvu utatoka ulimwenguni kote na watoto WOTE wa Mungu watapata miili yenye utukufu. Kile ambacho ni cha kuisha na ambacho pia ni cha kuharibika kitavalishwa sifa ya kutoharibika na ambayo itavikwa uzima wa milele.

Mabadiliko hayo yatakuwa ya ghafla na ya utukufu. Wakati huo ambapo Mungu atawafufua waliokufa pia atawabdalishwa watakaokuwa wakiishi ili wawe viumbe wenye uhai usioisha; na kupata miili ambayo haifi. Mwili wa wanadamu ambao ulikuwa dhaifu, na ambao ulivunja-vunjwa na maisha haya yanayoleta kifo cha kimwili, itafanywa kuwa miili ambayo ina nguvu ambayo tayari imebadilishwa na kufanywa upya.

Miili yetu ya sasa haiwezi kustahimili urembo na utukufu wa mahali ambapo Mungu ametuandalia pale mbinguni. Ndiposa Mungu ana mpango wa kutupatia mwili mwengine ambao utaweza kunawiri katika furaha ya kuishi milele huko Mbunguni. Miili hiyo iliyobadilishwa na ambayo itakuwa makao ya roho za milele haitawahi tena kunusa kifo. Lakini ni dhahiri kwamba Mungu aliamua kutodhirisha hali kamili ya mabadiliko ambayo yatafanyika, lakini ukweli ni kwamba mabadiliko hayo yatakuwa zaidi ya kile ambacho sisi wenywewe tunaweza kuelewa katika maisha ya kimwili ambayo tunaishi kwa sasa.

Basi wewe mwenzangu hebu jipe nguvu maishani haya, na hata wakati ambapo unapitia hali ngumu yenye uwezo wa kuleta mauti; wakati ambapo wewe mwenywewe utakuwa ukipitia bonde hilo la mauti au mtakapokuwa mkipita humo pamoja na mmoja wa wapendwa wako. Kama basi umeokoka na kutakaswa na damu ya Yesu basi kutakuwa na siku ambayo wewe mwenywewe utapata kubadilishwa. ■